

LICHA ya kuwa na ongozoko la bei za vyakula kwa viwango tofauti katika kata mbali mbali za Wilaya ya Mbarali, Wilaya hiyo imesema haina upungufu wa chakula kwa wakazi wake.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali ,Reuben Mfunne wakati akizungumzia hali ya chakula Wilayani humo na kusema kuwa wilaya hiyo ina chakula cha kutosha katika maeneo yake yote ya wilaya hiyo.

Mfunne anasema kuwa "kwa kata moja hadi nyingine debe moja la mchele kwa kata ya Ruiwa ni sh. 15,000/=, Madibira Sh. 18,000/=, Itambeleo (Kapunga) Sh. 20,000/=, Ipwani sh. 16,000/=, Mwatenga sh. 15,000/= na Lugelele sh. 17,000/=" alisema Mkuu huyo wa wilaya.

Hata hivyo Mkuu huyo wa Wilaya alisema kuwa kwa upande wa bei za sokoni ni kati ya sh. 1,400.00 – 2,000.00 kwa kilo.

Aidha Mfunne alisema katika wilaya hiyo hakuna utoro wa wanafunzi mashuleni unaotokana na ukosefu wa chakula katika kaya zao na kusema kuwa kwenye vituo vya afya hakuna wagonjwa waliobainika kuwa magonjwa yanayosababishwa na njaa.

Akielezea zaidi Mfunne alisema kwa ,msimu wa mwaka 2016/2017 wilaya ya Mbarali msimu imelenga kulima hekta 182,100 za mazao mbalimbali na matarajio ya mavuno ni tani 831,930.

Alisema mpaka februari 2017 ni jumla ya hekta 140,000 sawa na asilimia 75 zilikuwa zimelimwa na kupandwa katika maeneo ya mashamba makubwa ya Kapunga, Mbarali na Madibira pamoja na skimu nyingine 34 zenye miundombinu ya umwagiliaji iliyoboreshwa.

Hata hivyo Mkuu huyo wa Wilaya alisema kwa pamoja wamekuwa wakifanya ziara vijijini kuhamasisha na kuhimiza wakulima kulima mazao yanayokomaa mapema na yanayostahimili ukame pamoja na kutumia vizuri chakula kilichopo badala ya kukiuzwa kutokana na bei kubwa zilizopo.

“Nimekuwa nikiwashauri wafugaji kuuza mifugo waliyonayo kwa ajili ya kununua chakula badala ya kuendelea kukaa na mifugo mingi huku wakiwa hawana chakula katika familia zao” alisema Mfunne.

Alisema wilaya ya Mbarali kuna kaya wafugaji 7,369 za wafugaji zenye jumla ya ng’ombe 197,347, mbuzi 46,950 na kondoo 33,431 ambazo zimeelekezwa na kuhimizwa kuuza sehemu ya mifugo hiyo kwa ajili ya kununua chakula.

Aidha ukaguzi uliofanyika katika maghala 81 kipindi cha Januari, 2017 imebaika kuwepo kwa mpunga tani 39,131.9 na mchele tani 71 sawa na jumla tani 25,507 za mchele.